

BENKI KUU YA TANZANIA
16 Barabara ya Jakaya Kikwete
S. L. P. 2303
40184 DODOMA
TANZANIA

Simu: +255 26 2962586
Barua Pepe: botcommunications@bot.go.tz



BANK OF TANZANIA
16 Jakaya Kikwete Road
P.O. Box 2303
40184 DODOMA
TANZANIA

Phone: +255 26 2962586
Email: botcommunications@bot.go.tz

29 Juni 2021

TAARIFA KWA UMMA

HUDUMA ZA KIBENKI TAREHE 1 JULAI 2021

Tunapenda kuwajulisha kuwa usiku wa tarehe 30 Juni 2021 kuamkia tarehe 1 Julai 2021, Benki Kuu itakuwa inafunga **Mwaka wa Fedha wa Serikali na Benki Kuu**; hivyo, baadhi ya mifumo itasimama kuruhusu zoezi hilo la kufunga mwaka kukamilika.

Kutokana na hali hiyo, baadhi ya **huduma kama za kuhamisha/kutuma fedha kutoka benki moja kwenda benki nyingine** hazitakuwepo kwa **siku hiyo ya tarehe 1 Julai 2021**. Utaratibu huu si mgeni; huwa unafanyika kila mwaka tangu mwaka 2009.

Huduma zingine zote za ndani ya benki husika, zikiwemo za kuweka na kuchukua fedha kaunta na kwenye ATM zitaendelea kutolewa kama kawaida.

Utaratibu wa kawaida wa huduma utarejea tarehe 2 Julai 2021.

Benki Kuu inawashauri wateja wa mabanki kuwasiliana na benki zao kwa maelezo zaidi.

Imetolewa na:
Idara ya Uhusiano wa Umma na Itifaki